TANGAZO LA SERIKALI NA. 430 la tarehe 17/6/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA
(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHWAJI WA VIKUNDI VYA WATUMIAJI WA MAJI) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA, 2022

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishwaji wa Vikundi vya Watumiaji wa Maji) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka 2022, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Uanzishwaji wa Vikundi vya Watumiaji Maji) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 1029 ya tarehe 11/12/2020

2. Marekebisho yamefanyika kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza maneno yafuatayo katika tafsiri ya neno Mkurugenzi ***"pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi"***

Lakiri ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama uliofanyika mnamo tarehe…………Mwezi …………., 2022 na lakiri iliyogongwa na kushuhudiwa na:-

ASIA JUMA MESSOS,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya Mkalama*

JAMES JOHN MKWEGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Mkalama*

NAKUBALI,

**L.S**

INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB)
*Waziri wa Nchi-Or-Tamisemi*